USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

TOLEO NA. 5 • MEI-JULAI, 2018




## Uimarishaji Mifumo ya Rasilimali Watu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa

*Picha ya mbele: Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa wakiwa kwenye zoezi la uboreshwaji wa masijala ili kuondoa mrundikano wa majalada yasiyotumika, zoezi lililosimamiwa na OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na PS3 (Picha: Gladys Mkuchu).*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

USAID KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

UHURU NA UMOJA

# Bodi ya Uhariri


## Mwenyekiti

*Eng. Mussa Iyombe*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Charles Mhina – TAMISEMI*
*Mohammed Gombati – TAMISEMI*
*Ellen Mkondya-Senkoro – BMF*
*Rahel Sheiza – BMF/PS3*
*Josephine Kimaro – PS3*

## Waandishi

*Gladys Mkuchu – PS3*
*Jacqueline Sombe – PS3*
*Sylvia Kirenga – PS3*
*Elibariki Kanakoko – PS3*
*Zawadi Dakika – PS3*
*Damian Mwamongi – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Leah Mwainyekule – PS3*

## Wahariri

*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Nteghenjwa Hosea – TAMISEMI*
*Josephine Kimaro – PS3*
*Sylvia Kirenga – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Leah Mwainyekule – PS3*



## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blog: blog.tamisemi.go.tz*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri…………………………………………………………………………….uk 6**

**Mfumo Mpya Kusaidia Mgawanyo wa Watumishi Afya..…….…………….uk 8**

**Watumishi Afya Wafurahia Ahueni ya Kazi……….………………………uk 9**

**Watumishi Wapya wa Kigoma Watafutiwa Nyumba.……………………….uk 10**

**Watendaji wa Vijiji Bahi 'Wapigwa Msasa'………………..………………...uk 11**

**'Kwanini Nihame?'…………………………………………......…………….uk 12**

**Mipaka ya Kazi, Nidhamu Vyafundishwa Chunya………………………..uk 14**

**Serikali, PS3 Zaungana………...……………...…………………….………uk 15**

**Masijala Zafikiwa, Watendaji Wapigwa Butwaa...………...…………………uk 16**

**'Siri za Halmashauri Sasa Kutovuja Tena'…………………….…………....uk 17**

**Mwenyekiti Halmashauri Aahidi Ushirikiano Makete………..…….……...……uk 18**

**Mahojiano na Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu PS3……………….…uk 20**

**Utekelezaji Kazi za Rasilimali Watu katika Picha…………………...……..uk. 23**

*TAHARIRI:*

# Rasilimali Watu Imara ni Msingi wa Huduma Bora

Taasisi yoyote ile yenye maendeleo ni matokeo ya kuwa na Rasilimali Watu imara, wenye ari ya kutekeleza majukumu yao ili kuhakikisha kuwa dhima yao inasimamiwa na kutekelezewa kwa ufanisi. Usimamizi madhubuti wa Rasilimali Watu unachochea misingi imara ya uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) nchini, na kuhakikisha kuwa huduma bora zinatolewa kwa wananchi, hususani wale waliopo maeneo ya pembezoni ambayo ndiyo yenye uhitaji zaidi.

Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatambua mchango mkubwa unaofanywa na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kuhakikisha kwamba usimamizi wa Rasilimali Watu katika MSM na mifumo iliyopo inaboreshwa, ili kuweza kusaidia uwepo wa watumishi katika vituo vya kutolea huduma, hususani katika sekta ya afya na elimu.

Mdau mmoja wapo ni Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Tumeshirikiana na PS3 kwa karibu sana katika kuhakikisha kwamba mifumo ya Rasilimali Watu katika MSM zetu inaboreshwa. Hii inahusisha maeneo kadhaa, kama vile hatua za awali pale mtumishi anapopangiwa eneo la kazi na kusambazwa kwenye kituo cha kazi, na motisha kwa watumishi wa Umma.

*WISN* na *POA* ni mifumo muhimu katika kutambua vipaumbele vya watumishi kulingana na uhitaji, *WISN* inatoa taarifa kuhusu uhitaji wa watumishi kwa kituo, wakati *POA* hugawa watumishi kulingana na vipaumbele. Serikali na wadau imeweza kufanikisha mgawanyo mzuri wa watumishi katika MSM zetu, hasa kwa kuzingatia mahitaji ya kituo husika cha kutolea huduma. Hivi sasa maeneo yaliyofikiwa yameweza kuwa na idadi ya watumishi inaowahitaji, na kwingine kulikokuwa na mapungufu, nafasi hizo zimekuwa zikiendelea kujazwa.

Kwa kushirikiana na wadau, tumeweza kutumia mifumo iliyopo katika Wizara nyingine za kisekta, ili kupata taarifa muhimu juu ya uhitaji wa watumishi, na pia imewezesha kuwepo kwa kitini cha mafunzo ya awali kwa watumishi wapya wa MSM. Hii ni hatua muhimu ili kuwezesha watumishi kuwa na uelewa wa mazingira na matarajio ya mwajiri katika kutekeleza kazi zao.

Jambo lingine kubwa lililofanyika ni kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka. Tunafahamu kwamba masijala nyingi katika MSM zina nyaraka ambazo hazijawekwa katika mpangilio mzuri, jambo ambalo wakati mwingine linasababisha upotevu wa nyaraka muhimu. Hilo nalo limeanza kufanyiwa marekebisho, ili kusaidia katika kufanya maamuzi mbalimbali kupitia upatikanaji rahisi wa taarifa za mtumishi.

Jarida letu la safari hii linazungumzia kwa ujumla masuala yahusianayo ya usimamizi wa Rasilimali Watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM), na umuhimu wa kuwa na Rasilimali Watu iliyo imara kwa ajili ya maendeleo. Humu ndani utakutana na simulizi mbalimbali za watumishi walionufaika na uimarishwaji wa mifumo iliyopo, namna utendaji wao wa kazi ulivyobadilika, na wao kuwa na ari zaidi ya kufanya kazi, wakiamini kwamba wao ndio 'injini' ya mafanikio katika maeneo yao ya kazi.

Ushirikiano wetu ndani ya Serikali pamoja na nia ya dhati iliyopo na wadau wa maendeleo ndio uliofanikisha kwa kiasi kikubwa mabadiliko tunayoyaona leo. Ushirikiano huu unatakiwa kuendelea ili kuweza kuendelea kuboresha Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambazo ndizo zenye mawasiliano ya moja kwa moja na mwananchi. Bila kufanya kazi kwa ushirikiano, hatutaweza kufanikisha chochote.

Ni matumaini yangu kwamba kupitia jarida hili, wasomaji - hususan watumishi wa Umma - wataona namna gani wana mchango mkubwa katika kuleta maendeleo iwapo watatekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Vilevile, watajifunza namna MSM zinavyoweza kuja na njia mahususi za usimamizi wa Rasilimali Watu ikiwemo kutoa motisha ili kuhakikisha watumishi wanabaki katika vituo vyao vya kazi na utunzaji bora wa taarifa za watumishi ili kuboresha huduma zinazotolewa na MSM.


Nakutakia usomaji mwema!

**Eng. Mussa Iyombe**
**Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI**

# Usimamizi wa Rasilimali Watu katika Kuleta Maendeleo

Uimara wa taasisi yoyote unategemea uwepo wa Rasilimali Watu, hususani kwenye sekta ya Umma ambapo wao ndio msingi katika utoaji wa huduma. Taasisi za Umma zitaweza kutekeleza majukumu yake endapo zitaweka mikakati thabiti ya kuvutia, kuajiri, kusimamia na kuwabakiza watumishi wenye ujuzi kwenye nafasi zao kwa muda unaotakiwa. Usimamizi wa Rasilimali Watu ni msingi mkuu ambao una mawanda mapana na unaangalia mambo mbalimbali zaidi ya utoaji wa mishahara kwa watumishi.

Usimamizi wa Rasilimali Watu unajikita katika kuajiri na kuchagua watumishi wenye sifa na kwa idadi inayotakiwa; utoaji wa stahili, motisha na maslahi; usimamizi wa utendaji; mahusiano kazini; pamoja na mafunzo na maendeleo ya Rasilimali Watu ili kutoa fursa kwa wafanyakazi kuongeza ujuzi na utendaji kazi. Usimamizi huu unatazama pia maeneo yote yaliyotajwa hapo juu pamoja na kusimamia vipaji ili kuhakikisha kuwa malengo ya taasisi yanatimia. Usimamizi imara wa Rasilimali Watu imara katika mazingira yenye vikwazo vya kifedha na uhaba wa nguvu kazi inasaidia kukabiliana na changamoto hizo. Mifumo ya taarifa za Rasilimali Watu iliyo imara, jumuishi na inayoboreshwa mara kwa mara inasaidia kufanya maamuzi sahihi katika usimamizi wa idadi kubwa ya watumishi.




Mikakati jumuishi katika usimamizi wa Rasilimali Watu ni muhimu katika kusaidia watumishi kuweza kufanya kazi zao vizuri, kama inavyoonekana kwenye mchoro. Katika sekta ya utoaji huduma, hususani kwenye afya na elimu, kuwa na watumishi wenye ujuzi maalumu kulingana na vituo vyenye uhitaji huo ni muhimu sana katika kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa jamii. Mgawanyo sahihi wa watumishi katika shule na vituo vya afya nchini unahitaji uchambuzi yakinifu kwa kuangalia mahitaji kuanzia ngazi ya taifa, mkoa mpaka vituo vya kutolea huduma na kulinganisha na watumishi waliopo kwenye vituo ili kutambua uhaba uliopo. Katika mazingira ambayo kuna uhaba wa fedha na watumishi, maeneo yenye uhaba yaliyobainishwa yanatakiwa kupewa kipaumbele ili kuhakikisha kuwa watumishi wapya wanapelekwa maeneo yenye uhitaji zaidi.

Usimamizi wa Rasilimali Watu unatakiwa kwenda mbali zaidi ya kupeleka watumishi kwa kuhakikisha kuwa wanapewa ushirikiano ili kuweza kutekeleza majukumu yao. Watumishi wapya wanapaswa kupewa mafunzo ya awali, ikiwemo nini kinatarajiwa kutoka kwao (haki na wajibu) na pia nini watarajie kutoka kwa mwajiri katika kuwasaidia kutekeleza majukumu yao kama inavyotarajiwa. Hii inaenda sambamba na kutunza kumbukumbu za watumishi katika mpangilio mzuri ili waweze kupata stahiki zao kwa usahihi na wakati.

Taasisi zinapaswa kutoa ushirikiano na kufuatilia utendaji kazi wa watumishi kupitia mfumo mmoja wa upimaji wa utendaji kazi wa watumishi, pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha mazingira mazuri ya kazi ili kuwezesha watumishi kubaki katika vituo vyao vya kazi kwa muda unaotakiwa. Kwa maeneo ya mbali na miji, uwepo wa mipango maalumu ya motisha kulingana na mazingira husika ni njia sahihi zaidi. Mipango ya motisha inaweza kuwa ile ambayo haina gharama kubwa, motisha za kifedha, pamoja na kupatiwa nyumba na usafiri ili kusaidia watumishi kuishi kwa urahisi kwenye mazingira mapya.

Katika kuandaa mipango ya motisha kwa kuzingatia masuala mengine yote ya Rasilimali Watu, ni muhimu kuhusisha wafanyakazi. Mfumo mzuri wa usimamizi wa Rasilimali Watu unaelekeza na kusimamia mipango inayotekelezeka, na inatengenezwa kulingana na mazingira na kada zilizopo. Rasilimali Watu inatokana na mahitaji ya taasisi pamoja na yale yaliyobainishwa kutokana na kupima matokeo ya utendaji kazi. Vipengele vyote vilivyotajwa vya Rasilimali Watu na hatua zake vinahitaji kuwepo na mfumo thabiti wa taarifa za Rasilimali Watu.

Usimamizi wa Rasilimali Watu unaweza kuwa na changamoto mbalimbali na hakuna mbinu moja ambayo inaweza kutumika kwa watumishi wote au mazingira yote. Kuwepo kwa usimamizi mzuri wa Rasilimali Watu ni muhimu kwa mifumo imara katika sekta za Umma. Rasilimali watu sio tu muhimu katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora, lakini inaleta ufanisi wa nguvu kazi na kuchochea utendaji serikalini. Ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri na vituo vya kutolea huduma vina jukumu kubwa katika kuimarisha mifumo ya Rasilimali Watu Serikalini. Aidha, wadau wa maendeleo wanaweza kushirikiana na Serikali na kutoa mchango katika kuimarisha mifumo ya Rasilimali Watu.

*KUTOKA DODOMA:*

# Mfumo Mpya Kusaidia Mgawanyo wa Watumishi wa Afya

Licha ya idadi ya watumishi katika sekta ya afya kuongezeka katika miaka ya hivi karibuni, bado kuna changamoto ya upungufu wa watumishi hao, hasa katika maeneo ambayo ni magumu kufikika.

Katika juhudi zinazoendelea za kuboresha huduma za afya chini ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) pamoja na Mradi wa Uboreshaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), mipango mbalimbali inaendelea na kutekelezwa ili kuimarisha mfumo wa ugawaji wa watumishi.

Akiongea kuhusu mfumo wa ugawaji wa watumishi, Afisa Utumishi kutoka OR-TAMISEMI, Juma Mabrouk, anaeleza kwamba kwa sasa Wizara inashirikiana na Wizara ya Afya, Mradi wa PS3 na shirika lisilo la kiserikali la Touch Foundation kutumia mfumo wa *WISN* ambao unatoa taarifa kuhusu uhitaji wa watumishi kwa kituo, na mfumo wa *POA* ambao hugawa watumishi kulingana na vipaumbele.



***Afisa Utumishi kutoka OR-TAMISEMI, Juma Mabrouk, akichangia hoja katika mkutano wa wakufunzi na wataalam wa mfumo wa WISN plus POA uliofanyika mjini Morogoro (Picha: Jacqueline Sombe).***

"Kwa upande wa afya, tulikuwa na mwongozo wa miaka mitano wa mwaka 2014-2019 ambao ulikuwa ukitumika kama chombo cha kupanga watumishi. Mwongozo huu ulilenga kufanya ugawaji sawia wa watumishi, kwa maana kwamba idadi ya watumishi wapya ilikuwa sawa kwa kila kituo, bila kujali uhitaji, kwa vile tu vinafanana katika utoaji huduma," ameeleza Mabrouk.

Ameongeza kwamba mfumo huo haukuakisi uhalisia wa mazingira ya aina zote ya kufanyia kazi kwa wataalamu wa afya, kitu ambacho kilikuwa kinaleta changamoto katika ugawaji wa watumishi kwa kutumia mwongozo huo. "Lakini sasa kwa kutumia mfumo wa *WISN na POA*, tunagundua uhitaji wa eneo husika, na kupunguza idadi ya watumishi waliozidi, na kuwapeleka kwingine wanakohitajika," ameeleza Mabrouk.

Tofauti ya mfumo ambao ulikuwepo hapo awali kabla ya mfumo wa *WISN na POA,* anatanabaisha, ni kwamba mfumo huu mpya ni wa kielekroniki, wakati mwongozo ulikuwa si wa kielekroniki. Kutokana na mwongozo kutokuwa wa kielektroniki, haikuwa rahisi kujua uzito wa kazi kwa kada, kituo na Halmashauri na hivyo kusababisha watumishi kurundikana katika kituo kimoja, huku kituo kingine kikiwa na watumishi wachache.

Changamoto nyingine ambayo ilikuwa kwenye matumizi ya mwongozo ni kuchukua muda mrefu kufanya usambazaji, na kusababisha uwezekano wa mwingiliano wa maslahi binafsi; hii ikiwa na maana kwamba mwongozo hauna viwango vya udhibiti hivyo kuwa rahisi kuingilia na kuvuruga utaratibu mzima wa ugawaji wa watumishi.

Akieleza kuhusu matarajio mara baada ya kutumia *WISN na POA*, Mabrouk anasema: "Lengo kuu la mifumo ni kuboresha huduma za afya, kwani huwezi kuboresha huduma kwa wananchi bila kuwa na rasilimali watu itakayoweza kukidhi mahitaji ya watu."

*WISN na POA* itawezesha vituo vya afya kuwa na watumishi kutokana na uhitaji wa kazi husika. Pia utawanufaisha watumishi kupata muda wa kupumzika ili wasifanye kazi usiku na mchana. Vilevile, mfumo huu utasaidia watumishi kutochoshwa na mazingira ya kazi kwani hapo awali mtumishi alipaswa aingie zamu hadi mara mbili kwa siku ili kutoa huduma, lakini kwa kutumia mfumo huu mgawanyo wa kazi utakuwa sawia na usiochosha.

Kuhusu hatua ambazo zoezi hilo limefikia hadi sasa, Mabrouk amesema kwamba tayari wameshafanya ukusanyaji wa taarifa na kufanya mrejesho katika Halmashauri ambazo taarifa zimekusanywa.

Mikoa ambayo tayari zoezi hili limeshafanyika ni pamoja na Mara, Mwanza, Morogoro, Mbeya, Iringa, Kigoma, Tanga, Pwani na Mtwara.

***Na Jacqueline Sombe wa PS3***

## *KUTOKA MBEYA:*

# Watumishi Afya Wafurahia Ahueni ya Kazi

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Dkt. Marco Mbata, amesema matumizi ya mfumo wa kubainisha mahitaji ya watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuangalia uzito wa kazi *(WISN)*, sambamba na mfumo wa uchambuzi ili kubaini kada za kipaumbele zinazohitajika katika Halmashauri *(POA)* italeta unafuu wa kazi kwa watumishi wa Idara ya Afya.

Akizungumza wakati wa mahojiano, Dkt. Mbata amesema kwamba kwa kupitia mifumo hii, huduma katika vituo vya afya Rungwe itaboreshwa, kwani kutakuwa na idadi ya kuridhisha ya watumishi ambao watafanya kazi kwa zamu kama inavyotakiwa katika vituo vya afya nchini.

"Mifumo hii itaongeza sana motisha kwa watumishi waliopo kwa kuwa sasa idadi ya watumishi itaongezwa kutokana na mahitaji, hivyo mzigo wa kazi utapungua na kila mtumishi atakua anafanya kazi kwa kiasi na kupata muda wa kupumzika. Hali hiyo itawajengea watumishi hao faraja hivyo kujituma kwa kuona kwamba kazi yao imekua rahisi na inapewa kipaumbele," amesema Dkt. Mbata.

Akieleza changamoto walizokuwa nazo hapo awali katika Halamshauri ya Wilaya ya Rungwe, Dkt. Mbata anaeleza kwamba kabla ya kuwepo kwa mfumo hawakuwa na uwezo wa haraka wa kutambua uhitaji wa watumishi katika vituo vya afya Rungwe, na hapakuwa na uwezo mzuri wa kupima uzito ama wingi wa kazi kwa kitaalamu zaidi.

Naye Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Rebecca Msambusi, amesema kwamba mfumo huu wa *WISN na POA* utamsaidia yeye binafsi kama Afisa Utumishi, kwani unaweka pembeni suala zima la upendeleo wa kupeleka watumishi kutokana na kujuana na mtu.

Ameongeza kwamba mfumo huu pia utarahisisha sana kazi, kwani hapo mwanzo iliwachukua muda mrefu sana ukizingatia kwamba upangaji wa mwanzo haukuwa na vithibitisho, hivyo kuwazuia kufanya maamuzi. "Pia haikuwa rahisi kupima kazi, lakini kwa sasa hili ni tumaini kubwa sana kwetu kama Halmashauri," ameeleza.

Msambusi vilevile amesisitiza kwamba Rungwe ipo tayari na imejiandaa kuwapokea watumishi wapya ambao wameajiriwa hivi karibuni. "Nitahakikisha natumia mfumo wa *WISN na POA* kuhakikisha kila kituo kinapata watumishi kwa kulingana na uhitaji uliopo, na kuhakikisha kutumia kiongozi cha mafunzo ya awali kwa watumishi wapya ambacho kimeandaliwa na Serikali kwa kushirikiana na Mradi wa PS3," amesema.

Ili kutoa huduma bora kwa wananchi ambao ndio lengo hasa la Mradi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikishirikiana na PS3 imejikita kuwajengea uwezo Makatibu wa Afya, Wanganga Wakuu, na Maafisa Utumishi ambao ndio wahusika wakuu katika zoezi zima la upangaji wa watumishi katika vituo vya kazi ndani ya Halmashauri zao.



***Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Dkt. Marco Mbata, akitabasamu wakati wa mahojiano kuhusu mafunzo ya WISN na POA yaliyofanyika katika jengo la Hospitali (Picha: Jacqueline Sombe).***

Serikali pamoja na PS3 wameendesha mafunzo kwa watumishi wa umma waliopo katika Halmashauri za Mkoa wa Mbeya ili kuwajengea uwezo katika zoezi zima la kupanga watumishi kulingana na uzito wa kazi na mahitaji ya watumishi, na pia kuweka vipaumbele vya watumishi kulingana na kada ya afya.

***Na Jacqueline Sombe wa PS3***

## *KUTOKA KIGOMA:*

# Watumishi Wapya Kigoma Watafutiwa Nyumba

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma imepokea walimu wapya 93 wa Shule za Msingi. Walimu hawa wamehudhuria mafunzo elekezi kupitia Kiongozi cha Utaratibu wa Mafunzo Elekezi kwa Watumishi Wapya wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.



***Walimu wapya Arnold Patrick (kushoto) na Amina Abdallah wakiwa katika kituo cha kipya cha kazi, Shule ya Msingi Muungano iliyopo Kasulu, Kigoma (Picha: Zawadi Dakika).***

Katika kuweka mazingira bora ya kuwapokea watumishi hao wapya, uongozi wa Halmashauri ya Kasulu uliandaa kamati ya mapokezi ya walimu wapya, ambayo ilikua ikitoa maelekezo ya awali na kuwatafutia makazi ya muda.

Akisimulia mapokezi aliyoyapata, Mwl. Jordan Mwadeka wa Shule ya Msingi Makere aliyeajiriwa kutokea Mbeya, anasema: "Mapokezi na mafunzo elekezi niliyoyapata yameondoa dhana potofu niliyokuwa nayo kuhusu mkoa wa Kigoma. Awali nilidhani nisingeweza kufanya kazi huku kwa sababu ya umbali na mazingira, lakini kufuatia mapokezi niliyopata imekuwa rahisi sana kwangu."

Halmashauri nyingine iliyonufaika ni ya Wilaya ya Buhigwe, ambayo katika kipindi cha kuanzia Oktoba 2017 hadi Aprili 2018, imepokea watumishi wapya zaidi ya 50, 45 kati yao wakiwa ni walimu, na tisa wa Idara ya Afya ambao nao wamenufaika na mafunzo ya awali kazini.

Saratina Gesura ambaye ni muuguzi na mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo elekezi, anaeleza kwamba amefurahishwa sana na mapokezi katika kituo chake cha kazi, kwani amepata uelewa juu ya taratibu mbalimbali anazotakiwa kufahamu kama mtumishi mpya.

"Awali kulikuwa na changamoto pale watumishi wanapohama kwenda sehemu nyingine au kuripoti kwenye ajira mpya. Ilikuwa unafika wilayani lakini wahusika wa masuala ya utumishi hawatupokei vizuri, na ilikuwa ngumu kufahamu namna utakavyoweza kuishi. Lakini sasa imekuwa tofauti sana kutokana na mafunzo waliyotupatia juu ya utaratibu pale waajiriwa wanaporipoti kazini. Nashukuru kwa kuweza kupata mafunzo haya," amesema Gesura.

Gesura ameongeza kwamba walipokewa vizuri sana na ofisi ya Utumishi ya Halmashauri, kutafutiwa nyumba za kuishi, pamoja na kuelekezwa taratibu mbalimbali za ajira.

"Kipindi cha nyuma watumishi wapya walipata changamoto nyingi sana na wakati mwingine ilitwalazimu kuondoka mara tu wanaporipoti katika vituo vya kazi, kwa sababu wanashindwa kuelezwa taratibu za kazi na mazingira kwa ujumla," ameongeza Bi. Gesura.

Halmashauri tatu kati ya nane za mkoani Kigoma zimetoa mafunzo elekezi kwa watumishi wapya kwa kutumia Kiongozi cha Mafunzo ya Awali kwa Watumishi Wapya wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Utekelezaji huo unafuatia uzinduzi rasmi wa Mwongozo huo, na kupatiwa mafunzo pamoja na kusambazwa katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali mkoani Kigoma. Halmashauri hizo za Wilaya ni Kasulu, Buhigwe, na Uvinza.

Mwongozo huo umeandaliwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR- TAMISEMI), Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Utumishi), pamoja na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), ambao unashirikiana na Serikali ya Tanzania kuendesha mafunzo chini ya ufadhili wa Serikali ya Marekani.

***Na Zawadi Dakika wa PS3***

## *KUTOKA DODOMA:*

# Watendaji wa Vijiji Bahi 'Wapigwa Msasa'

Watumishi wengi wapya nchini Tanzania hawana uelewa mzuri juu ya haki, wajibu, sheria na kanuni za utumishi wa umma. Hii inatokana na taasisi zilizowaajiri kushindwa kutekeleza kikamilifu Waraka wa Utumishi Na. 5 wa Mwaka 2011 ambao unaelekeza watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza kupatiwa mafunzo elekezi ya awali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuajiriwa kwao.

Hali hii ilisababisha watumishi wengi kuingia katika utumishi wa Umma bila kuyafahamu maadili yanayoongoza utumishi wa umma, taaluma za kada zao, na kukosa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira ya kazi, hali ambayo imechangia sana katika kuathiri utendaji wa watumishi wa Umma, hasa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Rehema Madenge (kulia) akimkabidhi mmoja wa washiriki kitabu cha Kiongozi cha Utaratibu wa Mafunzo Elekezi ya Awali kwa Watumishi (Picha: Gladys Mkuchu).*

Kwe lengo la kuboresha utoaji huduma kwa wananchi katika Halmashauri zilizopo nchini, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), ikaona ni vema kuandaa Kiongozi ambacho kitatumika kutoa mafunzo kwa watumishi wapya ili kuboresha utendaji kazi wao.

Kiongozi hiki kimekuwa na manufaa hadi kufikia sasa, ambapo mkoani Dodoma, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi imekuwa mnufaika mkubwa kwa kutumia Kiongozi hicho kutoa mafunzo kwa watendaji wa vijiji wapatao 14.

"Tulikaa kwa siku nne na watendaji wapya 14 wa vijiji. Wakati wa mafunzo haya tuliweza kuwaeleza kila mmoja hali halisi ya eneo analokwenda kufanya kazi, na kila mmoja alipelekwa kwenye kituo chake cha kazi. Hii ilikuwa faraja kwani hawakutishwa na mazingira baada ya kupata mafunzo kama ilivyoelekezwa katika kiongozi hiki," anaeleza Bi. Faiza T. Nombo, aliyekuwa Afisa Utumishi Bahi. Bi Nombo hivi sasa amehamishiwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Bi Nombo ameeleza kuwa kwa upande wake yeye katika kutekeleza majukumu na kwa kuzingatia kiongozi cha mafunzo ya awali kwa watumishi wapya, alihakikisha watendaji wote 14 wanapata mapokezi mazuri, na walipokea mrejesho mzuri kutoka kwa watumishi hao baada ya kufika katika vituo vyao vya kazi.

"Mafunzo ndani ya kiongozi kwa watumishi wetu wapya yamekuwa ni rahisi na yanayoeleweka, na cha msingi zaidi yatawapa watumishi wetu wapya nafasi ya kuzingatia utoaji wa huduma bora kwa wapokeaji wa huduma hiyo. Ndani ya miezi miwili tuliweza kuona matokeo chanya na maboresho katika kuzingatia mahusiano na mawasiliano ya kikazi," ameongeza Bi. Nombo.

Bi. Nombo ameongeza: "Kwa maarifa ambayo nimeyapata kupitia kiongozi hiki, natamani kushirika ujuzi huu hata hapa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni niliyopo, ingawa haipo chini ya Mradi wa PS3."

Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa ambayo watumishi wapya wameweza kupata mafunzo kwa ajili ya kuwaandaa kwa majukumu yao, ambapo kiongozi hicho cha mafunzo ya awali kwa watumishi wapya wa MSM kilizinduliwa na aliyekuwa Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI mkoani Dodoma mnamo mwezi Julai 2017, na utoaji wa mafunzo ukaanzia hapo.

***Na Jacqueline Sombe wa PS3***

## *KUTOKA RUKWA:*

# 'Kwanini Nihame?'

### *Mpango wa motisha kwa watumishi Kalambo unavyowavutia kubaki katika vituo vya kazi*

Zile semi mbili za Waswahili *'Hayawi, hayawi, sasa yamekuwa'* na *'Mgeni njoo mwenyeji apone'* zimedhihirika baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa kuanza utekelezaji wa Mpango wa Motisha wa kupima na kukopesha viwanja kwa watumishi wake kwa lengo la kuongeza morali ya kufanya kazi.

"Nina miaka 10 katika Halmashauri hii. Hiki ni kitu kipya na kigeni kabisa katika Halmashauri. Sasa kwanini nihame? Una uhakika kinachotolewa huku (Halmashauri ya Kalambo) kiko huko (Halmashauri nyingine)?"

> *"Kwakweli hayawi, hayawi sasa yamekuwa. Vitu kama hivi tumevisubiri sana ."*

Hayo yalisemwa katika mahojiano maalumu na Akiba Goliamo, dereva wa Idara ya Utumishi na Utawala. Yeye ni mmoja wa wanufaika wa Mpango wa Motisha wa kukopeshwa viwanja na Halmashauri na kulipia kidogo kidogo kwa muda wa mwaka mzima.

Goliamo ametoa shukrani na pongezi nyingi sana kwa Halmashauri yake kwa kuja na mpango mzuri wa motisha ambao pia utaweza kuwainua watumishi kiuchumi kwa kuwa si watumishi wote wenye fedha taslimu ambao wangeweza kununua kiwanja kwa mara moja.

"Kwa njia hii ya malipo ya kidogokidogo basi inawezesha hata mtumishi wa chini kabisa kuweza kuhimili malipo na kuweza kumpunguzia mawazo kuhusu wapi atapata milioni mbili au tatu ili aweze kununua kiwanja kilichopimwa. Huu ndio utimilifu wa usemi *'mgeni njoo mwenyeji apone'* na sisi watumishi wa kima cha chini kwa hili tutapona tu," ameongeza.

Bwana Goliamo ameahidi kuendeleza eneo hilo mara tu atakapokamilisha malipo ya kiwanja hicho chenye ukubwa wa mita za mraba 1,700, huku akieleza kwamba atatumia kiwanja hicho kujenga nyumba yake ya makazi na sehemu iliyobakia itatumika kwa ajili ya kilimo cha bustani na ufugaji.

"Kwa kweli hayawi, hayawi sasa yamekuwa. Vitu kama hivi tumevisubiria sana," alisema kwa furaha mmoja wa watumishi ambaye hakupenda jina lake litajwe, alipokuwa akisoma tangazo la ukopeshwaji wa viwanja katika ubao wa matangazo wa Halmashauri.

"Upatikanaji wa viwanja ulikuwa mrahisi sana tena kwa bei nafuu sana, shida inakuja hujui eneo hili hapo baadae Halmashauri italitenga kuwa la biashara, makazi, barabara, hospitali, ya wazi, chuo au kituo cha mabasi," alisema, na kuongeza: "Heri kununua kiwanja ambacho tayari kimepimwa na Serikali kupitia idara husika ili kujinusuru na bomoa bomoa ya *Anko Magu*."

Hadi sasa viwanja vilivyopimwa na tayari kukopeshwa kwa watumishi ni 82, huku kila kiwanja kikiuzwa kwa bei elekezi ambayo ni mita moja ya mraba kwa shilingi za Kitanzania 1,000.

Awali Halmashauri hazikuwa na mipango ya motisha kwa wafanyakazi wake, hivyo Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) imekuja na mwongozo wa mpango wa motisha kwa wafanyakazi wa Halmashauri, na umeanza kutumika katika mwaka wa fedha 2017/18.



***Akiba Goliama ambaye ni mmoja ya wanufaika wa Mpango wa Motisha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo akiwa ametembelea eneo lake alililokopeshwa na Halmashauri (Picha: Elibariki Kanokoko).***

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Mhandisi Simon Ngagani, anasema kwamba mwaka 2016 watumishi wengi walikuwa wanaomba uhamisho, lakini baada ya kutangaza motisha mwaka 2017, maombi hayo ya uhamisho yalipungua.

"Unajua mtu akipata kiwanja anaendelea kuwepo, na akijenga nyumba ya kuishi ana uhakika kwamba ataishi hapo kwa muda mrefu," ameeleza, na kuongeza kwamba watumishi wengi wamechangamkia fursa hiyo na kujenga.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili, Richard Ngaita, ameeleza kwamba kwa kuona umuhimu wa watumishi, Idara ya Ardhi na Maliasili imeona ni vema kila mtumishi amiliki eneo kubwa na zuri.

***Inaendelea uk. 13***

## KUTOKA RUKWA:

# 'Kwanini Nihame?'

***Inatoka uk. 12***

Hivyo basi, amesema, mapendekezo ni mnunuzi kupewa kuanzia ukubwa wa mita za mraba 1000, ambayo itamgharimu shilingi milioni moja itakayomwezesha kumilika ardhi yake mwenyewe kwa kulipa kila mwezi kiasi cha shilingi 83,333 katika kipindi cha miezi 12.

Kwa kuongezea, Bwana Ngaita amewasihi watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kuchangamkia fursa hiyo kwani kwa maeneo kama Manispaa ya Sumbawanga mtu hawezi kupata kiwanja chenye ujazo mdogo *(low density)* kinachouzwa kwa shilingi milioni moja. "Kwa watumishi hii ni motisha tosha ukizingatia kwamba wananchi wengi kwa sasa nao wamefika kuulizia utaratibu wa kupata viwanja hivyo," amesema.

Hapo awali, Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo haikuwa na mpango mzuri wa motisha uliokuwa unatambuliwa kisheria katika Halmashauri, kwani mfumo uliokuwa unatumika kutolea motisha haukuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma ya ujazaji wa fomu za mfumo wa wazi wa mapitio na tathmini ya utendaji kazi (OPRAS).

> *"Laiti kama mambo hayo yote yaliyo kwenye mpango wa motisha yatawekwa kwenye utekelezaji, basi sidhani kama kuna mtu katika Halmashauri hii atatamani kuhamia Halmashauri nyingine."*

"Mfano mzuri ni utolewaji kwa zawadi za wafanyakazi bora katika Sherehe za Wafanyakazi. Wakati mwingine Mkuu wa Idara anakaa na wafanyakazi wake wanateua kwa utashi wao bila kuzingatia utaratibu maalum uliopo kisheria. Hivyo basi, mpango huu utasaidia kwanza kuboresha zawadi zinazotolewa kwa watumishi, lakini pia taratibu za utumishi zitatumika," ameeleza ndugu Joseph Chiwanga, Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala.

Mbali na hilo, mpango huu wa motisha ambao umepitishwa na Baraza la Madiwani mwezi Februari 2018 una malengo makuu matatu, ambayo ni kuongeza morali kwa watumishi, kuwavutia watumishi, na kuendelea kuwabakiza watumishi kukaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

Akiendelea na mahojiano, Ndugu Chiwanga amesisitiza kwamba azma ya Halmashauri ni kuhakikisha inaunga mkono juhudi Serikali ya awamu ya tano kuleta maendeleo, na hili litawezekana tu iwapo watumishi wa umma watawezeshwa kwa motisha itakayowawezesha kutoa huduma nzuri. "Je, namna gani ya kuongeza morali kama sio kwa kupata kiwanja ambacho thamani yake hupanda kila siku?" ameuliza.



***Afisa wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo akiangalia ubao wa matangazo ambao hutumiwa na Halmashauri hiyo kwa ajili ya matangazo ya manunuzi ya viwanja kwa watumishi. (Picha: Elibariki Kanakoko).***

Bwana Chiwanga ameongeza kwamba mpango huo utakuwa na utekelezaji kwa vipindi vitatu, ambapo hadi sasa wameanza na utekelezaji wa kupima na kukopesha viwanja, lakini pia tayari wameshaweka baadhi ya vipengele vilivyomo kwenye mpango katika bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2018/2019. Baadhi ya vipengele vilivyoingizwa kwenye bajeti hiyo ni kuboresha mazingira ya kazi, mfano ujenzi wa majengo ya shule, zahanati, ofisi za vijiji na kata, ukarabati wa nyumba za watumishi, kulipa madeni na stahiki za watumishi, ununuzi wa samani na mashine za kudurufu.

Mambo mengine ambayo yamepangwa kufanyika ili kuongeza morali kwa watumishi ni kupendekeza upandishwaji wa madaraja kwa wakati, pamoja na ununuzi wa pikipiki kwa watumishi walio mbali na vituo vyao vya kazi, au wenye mizunguko mingi ya kikazi.

"Laiti kama mambo hayo yote yaliyo kwenye mpango wa motisha yatawekwa kwenye utekelezaji, basi sidhani kama kuna mtu katika Halmashauri hii atatamani kuhamia katika Halmashauri nyingine," alisikika akisema mmoja wa watumishi kutoka Idara ya Uhasibu alipotembelea Ofisi ya Ardhi ili kupata utaratibu wa ukopeshwaji wa viwanja hivyo.

Mpango huo wa motisha umepangwa kuwa shirikishi kwa watumishi wote kutoa maoni yao ya nini kifanyike katika kuongeza morali ya kufanya kazi katika Halmashauri yao. Vilevile, Halmashauri inaandaa mikakati madhubuti kuhakikisha kwamba hata wale ambao wako mbali na maeneo ya awali yaliyopimwa wananufaika na mpango huo kwa kuhakikisha kwamba mazingira yao ya kazi yanaboreshwa zaidi, mfano uwepo wa vitendea kazi na mahali salama pa makazi.

***Na Elibariki Kanakoko wa PS3***

*KUTOKA MBEYA:*

# Mipaka ya Kazi, Nidhamu Vyafundishwa Chunya

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), imeandaa kiongozi cha mafunzo kwa watumishi wapya wa MSM ambacho kinawawezesha watumishi kupata maelekezo muhimu kabla ya kufika katika vituo vyao vya kazi.

Serikali ya Tanzania imejipanga kuongeza watumishi katika sekta mbalimbali, na ili ongezeko hilo la watumishi liweze kuwa na tija kwa Jamii, Serikali imeweka miongozo na mikakati madhubuti ya namna ya kuwasambaza watumishi hao ambao watajengewa uwezo kupitia kiongozi hicho. Kiongozi hicho kitamuongoza mtumishi ni kwa namna gani anatakiwa kutoa huduma katika kituo chake cha kazi.

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, ni moja ya Halmashauri nchini ambazo zimeshaanza kuona faida ya uwepo wa kiongozi hicho. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 watumishi 2058 wameajiriwa kufanya kazi katika zahanati na vituo vya afya mbalimbali hapa nchini. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya wahasibu watatu wameajiriwa kufanya kazi katika vituo vya afya.



*Mhasibu Msaidizi wa Kituo cha Afya Chalangwa kilichopo Chunya mkoani Mbeya, Joshua Green Mwalyengo, akieleza kuhusu mafunzo aliyopata. (Picha: Jacqueline Sombe).*

Akieleza kwa furaha, Joshua Mwalyengo ambaye ni mwajiriwa mpya kama Mhasibu Msaidizi katika Kituo cha Afya Chalangwa ni mnufaika wa mafunzo hayo, anasema kupata mafunzo kupitia kiongozi cha mafunzo kwa watumishi wapya kimemfanya kuelewa mambo mengi sana ambayo yatamwezesha kufanya kazi yake vyema.

> *"Mimi kama kijana mwenye ndoto za kufika mbali katika taaluma yangu, nitazingatia yale niliyojifunza..."*

"Nashukuru tangu niliporipoti kazini, tumekuwa na mafunzo ya wiki mbili yaliyoendeshwa na Pendo Ambokile ambaye ni mhasibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Halmashauri hii. Moja ya vitu ambavyo nimejifunza ni kuelewa taratibu za kazi, kuelewa majukumu yangu, mipaka ya kazi, nidhamu, pamoja na muingiliano wa majukumu," anaeleza Mwalyengo.

Mwalyengo anaendelea kuongeza kwamba kupitia utekelezaji wa kiongozi hicho ameweza kuelewa tamaduni za watu na Jamii katika kituo chake cha kazi.

"Mwongozo huu utanisaidia kuwa mtumishi mwenye maadili, mimi kama kijana mwenye ndoto za kufika mbali katika taaluma yangu, nitazingatia yale niliyojifunza kwa muda wa wiki mbili kupitia kitabu hicho ili niweze kufikia ndoto yangu," amesema kwa furaha.

***Na Jacqueline Sombe wa PS3***

## *KUTOKA LINDI:*

# Serikali, PS3 Zaungana Kuboresha Masijala Halmashauri

Kitengo cha Masijala katika Halmashauri nyingi nchini kimekuwa na changamoto katika utekelezaji wa majukumu yake ya uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka mbalimbali. Hii inatokana na kutofautiana kwa mifumo iliyopo ya uhifadhi na utunzaji nyaraka na kumbukumbu hizo.

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) pamoja na Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, zimeshirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), kuja na suluhisho. Baada ya kufanya tathmini na kupitia changamoto zilizopo katika Kitengo cha Masijala katika Halmashauri mbalimbali nchini, wameona umuhimu wa kuja na njia ya kutatua changamoto hizo kwa kila Halmashauri zilizopo katika mikoa 13 ambayo mradi unatekelezwa.

Akiwasilisha lengo la mpango huo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mkoani Lindi, Sylvia Kirenga kutoka Timu ya Rasilimali Watu PS3, amesema mpango huu una nia ya kuboresha Vitengo vya Utunzaji wa Nyaraka katika Halmashauri kutokana na uwepo wa changamoto mbalimbali za usimamizi na uendeshaji wa vitengo hivi.

"Kutotenganisha majalada ya watumishi baina ya yale ya siri na ya wazi ni baadhi ya changamoto tulizozibaini wakati wa tathmini. Tuligundua Halmashauri nyingi bado zinachanganya taarifa za siri na zile za wazi," amesema Kirenga.

Ameongeza kuwa majalada yaliyopo sasa siyo yanayotakiwa kutumika kulingana na mwongozo kutoka Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Imekuwepo changamoto ya rasilimali fedha katika uendeshaji wa masijali, hususan upatikanaji wa vifaa vya kufanyia kazi kama majalada, stempu, maboksi ya kuhifadhia nyaraka na mashubaka ya kuhifadhia majalada.

"Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imekuwa na changamoto mbalimbali katika Kitengo cha Utunzaji wa Nyaraka; mojawapo ni kuwa na vifaa duni na vilivyopitwa na wakati katika utendaji wa kazi zetu za kila siku. Tumekuwa tunatumia majalada ya zamani na tumekuwa tunachanganya taarifa za siri na za wazi katika jalada moja, ambapo ni kinyume na miongozo," amesema Jafarani Mkangumbe, Msimamizi wa Ofisi, Kitengo cha Nyaraka Ruangwa.

Ameongeza kuwa changamoto nyingine ni kutokuwa na sehemu maalum ya kuhifadhi majalada ambayo hayatumiki mara kwa mara na yale ambayo muda wake wa matumizi umepita, kama ya watumishi waliofariki au waliostaafu. Hii inasababisha mrundikano wa majalada yaliyo wazi na yale yaliyofungwa, hivyo kufanya utafutaji wa majalada yanayotumika kuwa mgumu.

"Tunaishukuru Serikali pamoja na PS3 kwa kuweza kuja na mpango huu wa kuboresha kitengo chetu, kwa kutukumbusha na kutupa mwongozo sahihi wa kutunza kumbukumbu. Tumeweza kupatiwa majalada mapya ya mfano na tumeweza kuhamisha taarifa za watumishi kulingana na mwongozo, yaani zile za siri na za wazi," ameeleza Mkangumbe.

Ametanabaisha kwamba wamepatiwa maboksi ya kuhifadhia majalada ambayo hayatumiki mara kwa mara, na hivyo wameweza kupunguza mrundikano wa majalada katika mashubaka. "Hii itaturahisishia sana kazi, hususani katika kutafuta majalada ya taarifa zinazotumika mara kwa mara," amemalizia.

***Na Gladys Mkuchu wa PS3***





*Kushoto: Mwangalizi wa Ofisi ya Kitengo cha Nyaraka katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Jafarani Mkangumbe, akiwa katika masijala wakati wa zoezi la kupunguza mrundikano wa majalada yasiyotumika. Kulia: Sylvia Kirenga, Meneja Uchambuzi kutoka Timu ya Rasilimali Watu PS3 akiwasilisha mada wakati wa kufunga zoezi la kuboresha masijala katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Lindi. (Picha: Gladys Mkuchu).*

*KUTOKA LINDI:*

# Masijala Zafikiwa, Watendaji Wapigwa Butwaa

Watumishi wa Kitengo cha Masijala katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, wamepigwa na butwaa kupokea ugeni kutoka Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, pamoja na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), waliotembelea Ofisi hiyo kuona hali halisi na utendaji kazi wa wataalam wa masijala, pamoja na kutoa mafunzo ya uboreshaji na uendeshaji wa Kitengo cha Masijala.

Akizungumza kwa hisia, Mtunza Kumbukumbu, Evodi Nyanda, amesema: "Yaani hii ni mara ya kwanza ugeni mzito kama huu kutembelea na kutoa mafunzo kwa watumishi wa masijala. Tumezoea kuona mafunzo yakitolewa kwa Idara zingine kubwa, lakini sisi hatujawahi pata hii fursa."

Ameendelea kusema kwamba mbali na mafunzo, hawajawahi kufanya maboresho yoyote, kuanzia mashubaka ambazo zilikuwa bado ni zile zile chakavu, na tena hazitoshi. "Majalada yalikuwa mpaka yanachanika yaani… kwakweli Masijala tumesahaulika kwa muda mrefu," ameeleza kwa hisia.

Akisimulia hali ilivyokuwa kwake binafsi, Nyanda anaeleza: "Nilikua napata mafua mara kwa mara kutokana na mrundikano wa majalada ambayo hayakuwa katika mpangilio mzuri kutokana na kukosekana kwa mashubaka. Naamini sasa ndio mwisho, na tutafanya kazi kitaalamu zaidi," ameyasema hayo akiwa anatembea kuelekea kwenye dawati lake ambalo kwa sasa baada ya maboresho, lina nafasi nzuri na uwazi wa kutosha.

Akiongea wakati wa mahojiano, Mtunza Kumbukumbu Msaidizi, Habiba Athumani, amezungumzia kukombolewa kwao na maboresho yaliyofanyika katika Kitengo cha Masijala. "Kweli mmetukomboa jamani; tumeufurahia mradi huu ambao umeikumbuka ofisi ya chini kabisa katika Halmashauri. Tumeongeza uelewa kupitia mafunzo mliyotupa na mmeboresha mazingira ya kazi na sisi sasa tumepata japo pa kuweka viti na meza zetu kwa nafasi," ameeleza kwa shauku.

Anatoria Anatory ni Mtunza Kumbukumbu kutoka Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Wakati akitoa mafunzo hayo, alisisitiza kwa uongozi wa Ruangwa kuhakikisha unatenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya masijala.

"Nyaraka ni lazima zifungwe, zirekodiwe na zihifadhiwe kwenye kituo maalum cha kuhifadhi kumbukumbu *'Records Centre',* hivyo ni muhimu wakati wote vitendea kazi viwepo ili kazi hii iweze kufanyika kwa ufanisi," amesisitiza.

Afisa Utumishi Mkuu pamoja na watunza kumbukumbu kwa pamoja wameishukuru Serikali pamoja na Mradi wa PS3, na kuiomba Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iwe tayari kutoa ushauri kila mara katika kuendelea kuboresha masijala ya Halmashauri hiyo.



***Afisa Kumbukumbu na Nyaraka kutoka Utumishi, Anatoria Anatory, akiwasilisha juu ya miongozo na taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Lindi (Picha: Gladys Mkuchu).***

Pia, wataalam hao wa masijala wamefurahishwa zaidi na mafunzo waliyopewa ya kupunguza mrundikano wa kumbukumbu *(decongestion)* ya majalada yaliyokwisha muda wake, kwani sasa imefanikisha upatikanaji wa nafasi ya kufanyia kazi zao za kila siku.

Masijala ni moja ya ofisi muhimu katika Halmashauri, lakini haikuwa inapewa kipaumbele katika kuimarisha utendaji wa shughuli za wataalam wa eneo hilo katika kupokea, kufanyia kazi na kuhifadhi nyaraka na barua zote zinazoingia na kutoka katika Halmashauri.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ambayo inasimamia Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, iliona umuhimu wa kuimarisha mfumo wa kutunza kumbukumbu za MSM, hivyo kushirikiana na Mradi wa PS3 kuboresha Kitengo cha Masijala katika Halmashauri na kuziwezesha kutunza nyaraka salama na kwa utaratibu stahiki.

Mradi wa PS3 ulishirikisha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, ili kuwezesha kazi ya kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika Halmashuari za Mikoa ambayo inatekeleza Mradi wa PS3.

***Na Sylvia Kirenga wa PS3***

## KUTOKA MBEYA

# 'Siri za Halmashauri Sasa Kutovuja Tena'





***Kushoto: Sanduku jipya la funguo mbalimbali za ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo; na kulia: kiboksi kilichokuwa kikitumika zamani (Picha: Mpigapicha wetu).***

Ni asubuhi yenye upepo mkali. Wingu la anga ni la kijivu, likionyesha kila dalili ya mvua kubwa kutaka kunyesha. Safari ya gari inaanza kwenye mji maarufu wa Tukuyu, na kukadiriwa kuchukua takribani dakika 60 kwa umbali wa kilometa 47 kutokana na hali ya barabara. Mvua inaanza kunyesha kwa nguvu na tope kuwa zito, huku wapita njia wakikimbia kujisitiri chini ya miti iliyoshamiri na kupendezesha mandhari kwa ukijani wake. Naam; mvua inaendelea na safari inaendelea, na kuishia moja kwa moja mbele ya nyumba ndogo yenye vyumba vitano hivi…hiyo ndiyo Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

Ikiwa imemegwa kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mwaka 2012, baada ya mlolongo wa mageuzi na hitaji la kutoa huduma bora na za kutosha kwa jamii, kitu cha kwanza utakachokigundua ukifika kwenye ofisi za Halmashauri Busokelo ni kisanduku kizuri kilichochongwa na kuning'inizwa ukutani kwa ajili ya kuhifadhi funguo. Miezi michache tu iliyopita, kisanduku hicho hakikuwepo.

"Ujue mwanzoni sanduku la funguo halikuwepo, na kiboksi tulichokuwa tunahifadhia funguo hakikuwa na usimamizi. Kila mtu aliweza kuchukua funguo wakati wowote na kuingia kwenye ofisi yoyote kuchukua au kusoma nyaraka za Serikali," anasimulia Robert Kipangule, Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

Tatizo hilo lilisababisha hata siri za Serikali kuvuja mara kwa mara na kuvuruga utaratibu mzima wa kazi na mipango ya Halmashauri, pia kuhatarisha usalama wa utendaji katika kufanya uamuzi na kushughulikia matatizo mbalimbali, anaeleza.

"Watumishi walikuwa wanapeleka siri za ofisi mpaka kwa wananchi. Kuna wakati mnapanga mipango ya kazi katika kata na vijiji, lakini utakuta wananchi wana habari kabla ya zoezi kufanyika na siku mnayofanya operesheni hiyo hampati kile mnachokitaka, kwa hiyo tunapoteza nguvu na rasilimali bila mafanikio," anasimulia Kipangule.

Hata hivyo, kwa sasa hali imebadilika.

Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka, pamoja na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR -TAMISEMI) na Mradi wa Uboreshaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), iliamua kufanya tathimini na kuja na mpango wa kuboresha masijala za Halmashauri, pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi wa masijala hizo.

Tathmini iliyofanywa ilibaini kuwapo kwa changamoto katika usalama wa kumbukumbu na nyaraka, mifumo ya utunzaji, na ufahamu wa watumishi wa masijala katika utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za Serikalini. Mpango huo wa maboresho ulienda sambamba na utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa masijala.

Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ni miongoni mwa Halmashauri zilizonufaika na mpango huo, na kwa sasa imewajengea uwezo watumishi wake wa masijala kutambua kuwa taarifa zote za Serikali zinakuwa salama, kwani ni nyenzo muhimu katika utendaji kazi wa Serikali.

Halmashauri hiyo pia ilikuwa inakabiliwa na changamoto ya watumishi wa masijala kutokuwa na ufahamu wa kutosha katika kuhifadhi na kutunza kumbukumbu, na hili lilichangiwa na kukosekana kwa mfumo sahihi wa kutunza na kudhibiti nyaraka, kwani masijala zao hazina mazingira yanayoruhusu utunzaji sahihi kutokana na miundombinu iliyopo kusababisha mrundikano mkubwa na kutokua na mpangilio maalum.

***Inaendelea uk. 19***

## KUTOKA NJOMBE:

# Mwenyekiti Halmashauri Aahidi Ushirikiano Makete

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Mhe. Egnatio Mtawa ameahidi ushirikiano katika zoezi la uboreshaji na uimarishaji wa masijala za siri na wazi za Halmashauri hiyo.

Mtawa ameyasema hayo wakati wa kikao cha mrejesho wa tathmini na mafunzo kwa timu ya menejimenti na watumishi wa masijala kuhusu usimamizi na uendeshaji wa masijala za siri na wazi katika Halmashauri.

Mhe. Mtawa ameishukuru sana Serikali pamoja na Mradi wa Uboreshaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), kwa kuja na mpango wa kuboresha masijala. "Kwa kweli hali iliyopo sasa ni mbaya na inahitaji uboreshaji wa haraka ili kuzisaidia Halmashauri kufanya kazi zake kwa weledi," amesema.

Kwa kuanzia, Kitengo cha Masijala kinahitaji bajeti ya kutosha kuboresha vitendea kazi, kisha kujenga uwezo wa wataalamu wanaohusika na eneo lile na baada ya hapo kuongeza usimamizi kwa watumishi wa masijala, ameeleza Mtawa, na kuongeza kwamba hilo litafanikisha watumishi kuwa waadilifu na wenye uwezo wa kutunza siri. "Kwa kufanya hivi kila kitu kitaenda sawa," amesisitiza.

Anna Msulwa ambaye ni Mtunza Kumbukumbu Msaidizi kutoka Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, akitoa mrejesho wa tathmini na mafunzo kwa watumishi wa Kitengo cha Masijala katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete, ameelezea kuhusu mafunzo kwa watumishi.

Watumishi walioainishwa wamepata mafunzo ya namna ya kufungua majalada ya siri na ya wazi, na namna ya kuyahifadhi, amefafanua, kama ilivyoelekezwa katika kitabu cha watumishi na watumiaji wa nyaraka *'Desk Instructions for Registry Staff and Records Users'* kinachoainisha utaratibu wa kufungua majalada.

Msulwa ameelezea umuhimu wa utunzaji wa jalada la siri la kila mtumishi na uwepo wa viambatanisho vyote muhimu vinavyohitajika, ikiwa ni pamoja na vyeti vya elimu, ndoa na kuzaliwa, barua ya ajira au mkataba, barua ya kupandishwa cheo, na nyaraka zote zilizoorodheshwa ndani ya jalada.

Amewaasa wasimamizi na watumiaji wa majalada juu ya matumizi ya *'minute sheet'* katika kila jalada na uandishi wake, ili kuwezesha kujua namna ambavyo nyaraka mbalimbali zilishughulikiwa mpaka mwisho wake.

Msulwa ameongeza kwamba tathmini ilionyesha watumishi wa masijala wanakosa sasisha (updates) za matumizi sahihi ya utunzaji kumbukumbu, kwani ufahamu na umakini wa nyakara zinavyotunzwa katika masijala hazizingatiwi.

"Kwa sasa utakuta majalada ya watumishi yaliyopo masijala ya wazi yanahifadhi nyaraka zote kwenye jalada moja (za siri na wazi); yaani hakuna tofauti ya kumbukumbu za wazi wala za siri. Hili haliruhusiwi. Baada ya maboresho haya hatutarajii kuliona tena kwenye utendaji kazi wetu wa kila siku," amesema Msulwa.

***Na Sylvia Kirenga wa PS3***



*Watumishi wa masijali Halmashauri ya Wilaya ya Makete mkoani Njombe wakimsikiliza Afisa Kumbukumbu kutoka Utumishi, Bi Anna Msulwa akiwaeleza matumizi ya majalada ya siri (Picha: Sylvia Kirenga)*

## KUTOKA MBEYA:

# 'Siri za Halmashauri Sasa Kutovuja Tena'

*Inatoka uk. 17*

Busokelo wao wakaamua wasiishie kwenye utunzaji wa mafaili tu, bali wadhibiti pia utunzaji wa funguo ambao ndio uliokuwa ukisababisha kwa kiasi kikubwa uvujaji wa siri. Waliamua kuboresha sanduku la kuhifadhi na kutunza funguo zote kwa kutafuta funguo mmoja utakaofungua sanduku zima, na mtu mmoja ndiye anayekaa na ufunguo huo.

"Dawa ya kudhibiti mianya ya watu kujipatia kirahisi taarifa za siri za Serikali katika Halmashauri yetu imegundulika na kudhibitiwa," anasema Kipangule na kuongeza: "Ofisi yangu itasimamia udhibiti na utunzaji ili kufahamu kama ufunguo umechukuliwa, kurudishwa na aliyeuchukua."

Naye Mtunza Kumbukumbu wa Halmashauri hiyo, Christina Mwaipopo, ameishukuru Serikali pamoja na PS3 kwa kuwajengea uwezo na kutambua wajibu wa watunza kumbukumbu kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo.

"Tulikuwa tunakabiliwa na changamoto kubwa ya kufuatilia na kutafuta taarifa kutokana na baadhi ya nyaraka kutokuwamo kabisa ndani ya majalada na mrundikano wa nyaraka, au jalada kuibiwa wakati linashughulikiwa ofisi nyingine," anaeleza.

Serikali pamoja na Mradi wa PS3 imetoa mafunzo kwa watumishi hao wa Halmashauri, pamoja na miongozo mbalimbali ya kudhibiti na kutunza kumbukumbu na nyaraka katika Halmashauri zote zinazotekeleza Mradi.

***Na Damian Mwamongi na Gladys Mkuchu wa PS3***



***Kushoto: nyaraka na majalada mbalimbali vikiwa vimehifadhiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, kabla ya kupata mafunzo ya namna ya kuhifadhi nyaraka na majalada (Picha: Mpigapicha wetu).***




***Kulia: Nyaraka zikiwa zimehifadhiwa vizuri kwenye maboksi baada ya mafunzo ya kuhifadhi nyaraka na majalada kufanywa katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo (Picha: Mpigapicha wetu).***

# Mahojiano Maalum na Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu PS3

**SWALI**: Wakati Mradi wa PS3 unaanza ilipita Halmashauri mbalimbali ili kuweza kutambua mahitaji kulingana na kada zilizopo. Mligundua nini?

**JIBU**: Mwanzoni tulishirikiana na Serikali katika kufanya utafiti ili kubaini mapungufu mbalimbali yaliyokuwepo. Tathmini ya Rasilimali Watu iliangalia maeneo mbalimbali yahusuyo usimamizi wa utendaji wa watumishi (OPRAS), upangaji wa Rasilimali Watu, na masuala ya kubakiza watumishi kwenye vituo vyao. Katika changamoto na mapungufu tuliyobaini, tumejikita hasa katika sekta ya afya na elimu, maana watumishi wengi wako katika sekta hizo, na hawa ndio wale ambao wanatoa huduma kwa karibu sana na wananchi. Mradi bado unaendelea na utafikia sekta zingine. Katika sekta hizi tumefanya kazi na wadau mbalimbali na kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukatumia mifumo iliyopo ya usimamizi wa Rasilimali Watu katika Halmashauri kwa lengo la kuboresha.

### Mafunzo ya awali kwa watumishi wapya

**SWALI:** Ni kwa namna gani PS3 imefanikiwa kuboresha mifumo ya usimamizi wa Rasilimali Watu tangu kuanza kwa mradi mpaka sasa?

**JIBU**; Katika hatua za mzunguko wa watumishi, cha kwanza kabisa ni kuajiriwa ambapo mtumishi anakwenda kuripoti katika kituo chake cha kazi. Ofisi ya Rais TAMISEMI na PS3 iliona ni jambo muhimu katika kuboresha utendaji wa kazi wa mtumishi ni kuwa na mafunzo ya awali kwa ajili ya watumishi wapya ambayo yatakuwa rahisi kwa kila mtumishi kupata pale atakapofika katika kituo chake cha kazi. Awali kulikuwa na mafunzo yaliyokuwa yanatolewa kwa ujumla pale wafanyakazi wapya wanapofika na kukaa darasani kwa siku mbili hadi tano na baada ya hapo hakuna tena mafunzo yanayoratibiwa vizuri na endelevu katika sehemu zao za kazi.

Kwahiyo OR-TAMISEMI iliunda kikosi-kazi kwa ajili ya kutengeneza Kiongozi cha Mafunzo ya Awali kwa Watumishi Wapya wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia taratibu za kisera na miongozo mbalimbali ya Serikali.

**SWALI**: Nini faida za kuwa na kiongozi hiki?

**JIBU**: Lengo kuu la kitini hiki ni kuchangia katika kubakiza watumishi wapya katika vituo vyao vya kazi. Kiongozi hiki kimetengenezwa ili kupunguza gharama ambazo Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) zilikuwa zinaingia hapo awali katika kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi. Kwa sasa mtumishi anapata mafunzo palepale Halmashauri anapofika, na pia katika kituo chake cha kazi, hivyo MSM haihitaji kukusanya watumishi kutoka maeneo mbalimbali mahala pamoja kwa ajili ya kutoa mafunzo.



*Mkuu wa Timu ya Rasilimali Watu PS3, Dkt. Josephine Kimaro wakati wa mahojiano na mwandishi wa makala hii (Picha: Jacqueline Sombe).*

Mafunzo ya awali kwa watumishi yalilenga kuangalia mambo kadhaa ya kiutumishi na maadili, lakini hakukuwa na utaratibu mahususi wa kutoa mafunzo ya kitaaluma katika kituo cha kazi. Kiongozi hiki kinatoa nafasi na maelezo kwa wakuu wa idara mbalimbali katika MSM kuhusu mafunzo ya msingi ya kitaaluma. Kwa mfano, mtumishi wa sekta ya kilimo anaporipoti katika Halmashauri, Mkuu wa Idara ya Kilimo inabidi akutane naye na kumpa mambo ya msingi ya kisekta, changamoto zilizopo, na jinsi ya kuzitatua. Mtumishi huyo huyo anapofika katika ngazi ya kata na kijiji atapata mshauri (mentor) atakayempa maelekezo ya kitaaluma kwa vitendo, mfano kama vile kutembelea mashamba kwa kipindi cha miezi sita.

Faida nyingine ya kiongozi hiki ni kutoa nafasi na kuainisha majukumu kwa wadau mbalimbali waliopo katika Halmashauri, kata, vijiji pamoja na kituo cha kazi. Kiongozi vilevile kinaainisha majukumu ya jamii, ikiwemo jinsi ya kutatua changamoto za makazi kwa ajili ya watumishi wapya na jinsi wanavyotakiwa kuwapokea.

### Mgawanyo wa watumishi

**SWALI:** Kuna changamoto gani katika usimamizi wa watumishi, hususani mgawanyo wa watumishi katika MSM kulingana na vituo vya kutolea huduma pamoja na vipaumbele kulingana na kada na uhitaji?

**JIBU**; Changamoto iliyopo katika usimamizi wa watumishi ni pamoja na upatikanaji wa watumishi, idadi yao, na eneo wanakoenda kufanyia kazi. Aidha kuna changamoto ya uwiano wa watumishi katika maeneo mbalimbali. MSM inakabiliwa na changamoto ya uwepo wa watumishi wengi katika vituo vya mjini kuliko vya pembezoni. OR-TAMISEMI, Wizara ya Afya, na PS3 zimepitia katika hatua mbalimbali za kutatua changamoto hii, hususani katika sekta ya afya, ili kuhakikisha kwamba watumishi wanaoajiriwa wanasambazwa katika sehemu zenye uhitaji zaidi.

***Inaendelea uk. 21***

# Mahojiano Maalum na Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu PS3

*Inatoka uk. 20*

**SWALI**: Mmewezaje kutambua maeneo yenye uhitaji zaidi na kuzipa vipaumbele?

**JIBU**: OR-TAMISEMI, Wizara ya Afya, PS3, na shirika la Touch Foundation, zimeshirikiana katika kutumia mfumo wa WISN na POA ili kuweza kubaini mahitaji na vipaumbele vya watumishi wa sekta ya afya katika MSM. Mfano, unapopata watumishi kumi na kujiuliza wanahitajika kupelekwa katika vituo gani vya afya, basi mifumo hii inatambua uzito wa kazi kwa kada, na vituo vya afya vya Halmashauri nzima. Hivyo basi, watumishi wapya watapelekwa katika maeneo yenye uhitaji zaidi kulingana na uzito wa kazi na huduma zinazotolewa. Ukiangalia katika vituo vya afya, kiwango cha huduma zinazotolewa hakifanani. Kwa mfano, kuna akina mama wanaokuja kujifungua, vilevile kliniki ya watoto na huduma zingine ni tofauti kutoka kituo kimoja hadi kingine, na hiyo ndiyo inayoonesha uzito wa kazi na vipaumbele vya mahitaji ya watumishi kwa idadi na kada.

**SWALI**: Taarifa hizi mnazipataje ili kuwezesha utendaji kazi wa mifumo hii miwili?

**JIBU**: Kwa sasa taarifa hizi zinapatikana kutoka katika mfumo wa DHIS2 ambao unabeba taarifa za huduma za vituo vya afya na Halmashauri kwa ujumla. Faida mojawapo ya kutumia taarifa zinazotoka kwenye DHIS2 ni kusaidia MSM ziweze kujitegemea katika kuandaa taarifa za mahitaji ya watumishi wa sekta ya afya kwa kutumia taarifa ambazo wanazo. Taarifa zinazotoka kwenye mfumo huu si tu kwamba zitasaidia kusambaza watumishi kwa vipaumbele vilivyopo, bali itasaidia pia MSM kuandaa makisio ya watumishi wanaohitajika yenye uhalisia zaidi kila mwaka.

### Kuwabakiza watumishi katika vituo vyao vya kazi

**SWALI:** Serikali na PS3 zimesaidia kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wapya na kuweza kutambua uhitaji wa watumishi katika MSM. Ni mikakati gani inatumika kuhakikisha watumishi hawa wanaendelea kubaki kwenye vituo vyao vya kazi?

**JIBU:** Kuna mbinu mbalimbali za kuwawezesha watumishi kubaki kwenye vituo vyao vya kazi, njia kuu ikiwa ni kuwapa motisha ya kifedha na isiyo ya kifedha watumishi wa Halmashauri. OR-TAMISEMI, OR-Utumishi na PS3 zilishirikiana kufanya utafiti ili kubaini namna ambavyo MSM zinatoa aina mbalimbali za motisha kwa watumishi. Ilibainika kwamba zipo changamoto mbalimbali katika utoaji wa motisha, ikiwemo gharama kubwa inayohitajika, na kukosekana kwa mbinu mbalimbali za utoaji wa motisha. Kulingana na mazingira ya Halmashauri husika.



*Mkuu wa Timu ya Rasilimali Watu PS3, Dkt. Josephine Kimaro (Kushoto mwisho) akiwa katika majadiliano na wadau wa Rasilimali Watu mjini Morogoro (Picha: Maktaba)*

> *"Baadhi ya Halmashauri zimepanga kutoa au zimetoa usafiri kama baiskeli na pikipiki kuwawezesha watumishi kufika sehemu zao za kazi kwa urahisi na haraka."*

Kwahiyo OR-TAMISEMI, OR-Utumishi, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, pamoja na PS3 zilishirikiana katika kutengeneza utaratibu wa kutengeneza mikakati ya utoaji wa motisha kwa MSM. Mambo ambayo tumekubaliana ni pamoja na kuangalia vitu gani vidogo ambavyo viko ndani ya uwezo wa Halmashauri na vitaweza kuwa motisha kwa watumishi kulingana na utendaji wa kazi, mahitaji yaliyopo, na changamoto za kimazingira.

Katika utekelezaji wa mikakati hii, baadhi ya MSM zimetengeneza mipango ya kutoa motisha kwa wafanyakazi ili kuwapa morali na kubaki kwenye vituo vyao vya kazi. Kwa mfano, baadhi ya Halmashauri zimepanga kutoa, au zimetoa usafiri kama baiskeli na pikipiki kuwawezesha watumishi kufika sehemu zao za kazi kwa urahisi na haraka. Baadhi ya Halmashauri zimekuja na ubunifu wa kutoa ardhi kwa watumishi kama motisha, ili kubakiza watumishi na kuongeza ufanisi wa kazi.

### Utunzaji Nyaraka na Kumbukumbu

**SWALI:** PS3 imeshiriki katika kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na masijala katika MSM. Ni kitu gani kimepelekea kutekeleza hili?

**JIBU:** OR-TAMISEMI, Ofisi ya Rais - Idara ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (PORAMD), Sekretarieti za Mikoa na PS3 zimeshirikiana katika kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za kiutumishi katika MSM. Tulikubaliana kufanya zoezi hili kwa njia ya kutoka chini kwenda juu (bottom-up approach). Utaratibu huu uliwezesha MSM kubaini changamoto na mahitaji yaliyopo katika utunzaji wa kumbukumbu. Pia tulitaka kujenga umiliki na uimara wa zoezi.

*Inaendelea uk. 22*

# Mahojiano Maalum na Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu PS3

*Inatoka uk. 21*

**SWALI:** Halmashauri zimebaini changamoto zipi na mahitaji yapi ili kusaidia kuboresha utunzaji wa kumbukumbu zao?

**JIBU:** Changamoto zinazotajwa na MSM ni pamoja na masijala zisizotosheleza na hivyo kusababisha mrundikano wa majalada ya taarifa hasa za utumishi. Hii hupelekea MSM kutumia muda mrefu katika kupata taarifa na kutoa maamuzi ya mtumishi kwa wakati. Wakati mwingine, mtumishi anasafiri kuja Halmashauri kupata taarifa zake lakini hutumia muda mrefu na kumlazimu kukaa zaidi ya siku moja ili aweze kutafutiwa jalada lake, hivyo kuathiri utoaji wa huduma. Aidha, changamoto hii huweza kupelekea kukosekana kwa taarifa zote za mtumishi husika, na kumuathiri katika utumishi wake hadi anapostaafu.

Changamoto nyingine ni kutokuwa na vitendea kazi, kama vile majalada yanayotunza taarifa za mtumishi (master files). Kila mtumishi anatakiwa kuwa na jalada moja kuu lenye kuorodhesha taarifa zake zote za utumishi, lakini hii haifanyiki katika Halmashauri nyingi na hivyo kufanya zoezi la rejea za taarifa za watumishi kuwa ngumu kuzipata pale zinapohitajika.

**SWALI:** Nini kimefanyika ili kuwezesha mafanikio ya uboreshwaji wa utunzaji wa kumbukumbu, na mafanikio ni yapi?

**JIBU:** Ili kufanikisha zoezi, OR-TAMISEMI, PORAMD, Sekretarieti za Mikoa na PS3 tulienda katika Halmashauri mbalimbali na kujenga uelewa wa utunzaji wa kumbukumbu. Aidha, timu ya wataalam wa utunzaji wa kumbukumbu ilishirikiana na MSM katika kupanga masijala za Halmashauri ili kuondoa mrundikano wa majalada. Mabadiliko mengine ni kuwa tumeweza kuwajengea uwezo watumishi wa masijala kwa kuwaeleza miongozo mbalimbali ya namna ya kutunza kumbukumbu, na wengi wamefurahia na wamekiri kuona faida ya mafunzo hayo.

**SWALI:** PS3 kupitia eneo la Rasilimali Watu kwa ujumla imewezaje kuhakikisha kuwa dhima ya mradi ya kuboresha mifumo ya sekta za umma katika kuhakikisha kuwa wananchi wenye uhitaji wanapata huduma bora inafikiwa?

**JIBU:** Hakuna taasisi inayoweza kufanikiwa bila kuwa na Rasilimali Watu, lakini wanatakiwa wawe kwa idadi na taaluma zinazotakiwa, pamoja na morali ya kufanya kazi. Kuwepo kwa uimara wa Rasilimali Watu katika MSM ambazo ndio zinafanya kazi karibu kabisa na wananchi kupitia vituo vya kutolea huduma, kutachochea utoaji wa huduma bora kwa wananchi.



*Mkurugenzi wa Programu wa taasisi ya Benjamin Mkapa (BMF) ambao ni wadau wa PS3, Rahel Sheiza, akiwasilisha mada kuhusiana na mipango ya motisha ya MSM kwa mkoa wa Mwanza (Picha: Maktaba).*

Iwapo kuna vituo vingi vya kutolea huduma na hakuna Rasilimali Watu wenye taaluma zinazohitajika, itakuwa ni kazi bure. Mfano, kuwe na kituo cha afya bila kuwa na mkunga mwenye taaluma, itasababisha kudorora kwa huduma ya mama mjawazito, na vifo vya mama na mtoto kuongezeka. Lakini kuwepo kwa mtumishi mwenye taaluma kutachochea huduma bora kwa wananchi wenye uhitaji.

**SWALI:** Je, PS3 ina mpango wowote wa kuboresha Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Rasilimali Watu?

**JIBU:** Taasisi yoyote, hususani zenye watumishi wengi kama Serikali, zinahitaji kuwa na mfumo wa taarifa wa usimamizi wa Rasilimali Watu unaobaini watumishi katika vituo vyao vya kazi, pamoja na taarifa zingine ili kuchangia ufanisi katika upangaji wa watumishi na utoaji wa maamuzi ya kiutumishi kwa wakati. Serikali zinahitaji mfumo ambao utabeba majukumu yote na kwa usahihi kuhusu usimamizi wa Rasilimali Watu kuanzia ajira, upimaji wa utendaji, maslahi na motisha, na ukomo wa ajira ya mtumishi. Pamoja na mambo mengine, mfumo wa taarifa za Rasilimali Watu unaweza kubadilishana taarifa na mifumo mingine kwa ajili ya kuongeza ufanisi na utoaji wa maamuzi kwa wakati. PS3 inaipongeza Serikali kwa kuanzisha, kuusimamia na kufanya maboresho ya mfumo wa Human Capital Management Information System (HCMIS) tangu ulipoanzishwa. Aidha, PS3 imeona nia ya dhati ya Serikali katika kuendelea kufanya maboresho yenye kuongeza tija na ufanisi. Tunaendelea kufanya majadiliano na Serikali, na Mradi una nia ya kushirikiana katika kuimarisha zaidi mfumo wa HCMIS kulingana na mahitaji yaliyopo ili kutatua changamoto zilizopo za mfumo huu wa taarifa za Rasilimali Watu.

***Na Gladys Mkuchu wa PS3***

## *UTEKELEZWAJI WA KAZI ZA RASILIMALI WATU KATIKA PICHA:*



***Katibu wa Afya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Faraja Mdendemi, akionyesha jinsi mfumo wa WISN na POA unavyofanya kazi, mara baada ya kupata mafunzo katika Halmashauri hiyo.***




***Afisa Utumishi wa OR TAMISEMI, Elias Magere (kushoto), na Katibu Muhtasi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa wakishiriki zoezi la uboreshwaji wa majalada ya taarifa za watumishi.***



***Mmoja wa wawezeshaji, Fabain Gapchojiga, akifanunua jambo kwa washiriki wa mafunzo ya motisha kwa wafanyakazi wa Serikali yaliyofanyika mkoani Morogoro.***



***Mkufunzi wa kitaifa wa WISN plus POA, Charles Makama (katikati) akitoa mafunzo kwa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Kushoto) ni Afisa Utumishi wa Rungwe, Rebecca Msambusi, na kulia ni Katibu wa Afya.***




***Mkurugenzi wa Mradi kutoka shirika la Touch Foundation, Valerio Parisi, akitoa mada katika mkutano kazi wa timu ya wataalam wa WISN na POA uliofanyika mkoani Mtwara.***



***Washiriki wa mafunzo ya motisha kwa watumishi kutoka Halmashauri za mkoa wa Morogoro wakifuatilia mada wakati wa mafunzo hayo mkoani humo.***

# MIFUMO YETU